

Multicultural Policy for the Northern Territory 2020-25 Fact Sheet

Karatasi la Ukweli, la Sera za Kitamaduni tofauti, la Wilaya ya Kaskazini, Mwaka wa 2020-2025

Sera za kitamaduni tofauti za Wilaya ya Kaskazini 2020-25 zinatambua nguvu na mchango mzuri wa tamaduni nyingi katika maendeleo ya maisha yetu ya kijamii na kiuchumi katika Wilaya ya Kaskazini.

Sera za kitamaduni tofauti zinaweka mikakati ya kujenga, kuimarisha na kuunga mkono matokeo mema ya mhamiaji na jamii zenye tamaduni tofauti katika Wilaya ya Kaskazini. Inakuza ushirika wenye nguvu, ushiriki ulioimarishwa na jamii zenye tamaduni tofauti na inachangia katika masomo, kusherehekea na ushirikiano wa tamaduni tofauti.

Kanuni zinazoendeleza sera za kitamaduni tofauti ni kama vile:

- Kuthamini utofauti wetu
- Kusaidia upatikanaji
- Kuhakikisha ushiriki na ujumuishaji
- Kuimarisha heshima na mshikamano ya kijamii.

Malengo hayo manne makuu ya sera za kitamaduni tofauti yametegezwa kuhakikisha matokeo mema ya mhamiaji, na jamii zenye tamaduni tofauti katika Wilaya ya Kaskazini ni pamoja na:

- **Kujenga utofauti wetu kwa** kusaidia idadi ya watu wenye tamaduni tofauti katika Wilaya na kukuza makaazi katika Wilaya ya Kaskazini.
- **Kuimarisha ushirikiano wetu** na wadau mbalimbali, kwa kuhakikisha watu kutoka katika jamii zenye tamaduni tofauti wanapokea huduma na usaidizi wanaohitaji
- **Kusaidia Kushiriki, Ujumuisho wa Kijamii na Ushikamano katika jamii yetu** ili kuwezesha jamii zenye tamaduni tofauti kujihusisha katika vipengele vyote vya maisha Wila yani Kaskazini, ikijumuisha pamoja na ajira.
- **Kuimarisha jamii yetu** kupitia ujenzi wa uwezo, kukuza heshima ya pande zote na kuwezesha masomo, kusherehekea na ushirikiano wa tofauti zetu za tamaduni.

Hatua muhimu za sera za kitamaduni tofauti zimeundwa katika mipango ya kisasa na misaada ya kifedha, pamoja na mipango na sera katika afya, elimu na makaazi.

Sera za kitamaduni tofauti pia zinahusisha hadithi za wahamiaji ambao wameifanya Wilaya ya Kaskazini kuwa makao yao, na mashirika ya kijamii ambayo yamechangia idadi yetu yenye tamaduni tofauti.

Nakala ya sera za kitamaduni tofauti ya Wilaya ya Kaskazini 2020-25 inapatikana katika mtandao <https://territoryfamilies.nt.gov.au/policy/multicultural-affairs>

